JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UWEKAJI WA VITU VISIVYO CHAKULA KWENYE BAADHI YA BIDHAA ZA CHAKULA ZILIZOFUNGASHWA

**Dar es Salaam, 16 Agosti 2025.**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuutarifu umma kuwa kupitia kaguzi zilizofanyika katika soko lilibaini kuwa kuna baadhi ya wazalishaji wanaozalisha na kusambaza bidhaa za chakula pasipo kuzingatia Kanuni Bora za Uzalishaji (*Good Manufacturing Practices*) pamoja na Kanuni Bora za Usafi (*Good Hygenic Practices*) ambapo huweka vitu visivyo chakula ndani ya baadhi ya bidhaa za chakula kilichofungashwa kama zawadi ili kuvutia walaji hususan watoto.

Shirika lilichukua hatua ya kuziondoa bidhaa hizo katika soko na kuwataka wahusika kutoendelea kuzalisha, kuingiza au kusambaza bila kufuata utaratibu kwani kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Sura 130 na Kanuni zake, hairuhusiwi vitu ambavyo si chakula kufungashwa pamoja na chakula ili kulinda afya ya walaji.

Hivyo, Shirika linapenda kutoa agizo kwa wazalishaji, waingizaji na wasambazaji wa bidhaa husika kuziitisha na kuziondoa kwenye soko (*recall*) mara moja. Shirika linaendelea kufanya kaguzi za ufuatiliaji katika soko na kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha wahusika wanaoendelea kukiuka taratibu za usalama na ubora wa bidhaa za chakula wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, Shirika linatoa wito kwa umma kutoa taarifa kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800 11 0827,** ofisi ya TBS iliyo karibu nao au ofisi ya Halmashauri pindi wanapobaini uuzaji wa bidhaa za aina hizo.

**Imetolewa na:**

Gladness H Kaseka
**Meneja wa Uhusiano na Masoko**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na: +255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na: +255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na: +255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na: +255 28 2804023